**5.0 MAMLAKA YA KUKAGUA NA KUKAMATA MALI IDHANIWAYO NI ZAO LA UHALIFU.**

Sheria ya Mazao ya Uhalifu, imewapa mamlaka Jeshi la Polisi la ;

- kukagua na kukamata mali yoyote inayodhaniwa kutumika kufanya uhalifu au ni zao la uhalifu kwa kufuata taratibu za kisheria;
- kuomba benki au taasisi ya kifedha kufungia akaunti ya mteja inayodhaniwa kupokea fedha zitokanazo na uhalifu; na
- kuchunguza akaunti inayodhaniwa kupokea fedha zinazotokana na uhalifu .

**6.0 KURUDISHWA KWA MALI INAYODHANIWA NI ZAO LA UHALIFU.**

Mali iliyokamatwa kama zao la uhalifu inaweza kurudishwa kwa mhusika kama masuala yafuatayo yatabainika;

- kukosekana kwa ushahidi wa kuunganisha mali hiyo na uhalifu,
- hakuna kesi iliyofunguliwa mahakamani kuhusu mali hiyo; au
- hakuna amri ya mahakama kutaifisha mali hiyo.

**7.0 HITIMISHO**

Wahalifu wamekuwa wakitumia mbinu mbalimbali kuficha faida zinazopatikana kutoka kwenye uhalifu, hivyo kutaifisha mazao ya uhalifu ni muhimu katika kuzuia uhalifu mwingine kutendeka lakini pia kuikumbusha jamii kuwa uhalifu hauna faida.


**Kwa Maoni, wasiliana na Tume kupitia anuani ifuatayo :**

**Katibu Mtendaji,**
**Tume ya kurekebisha Sheria Tanzania ,**

**Jengo la Taaluma Na. 1,**
**Barabara ya Mkalama**
**S.L. P 1718**
**DODOMA**
**TANZANIA**

**Barua pepe: lrct@lrct.go.tz**
**Tovuti: www.rlct.go.tz**


**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA

# MAZAO YA UHALIFU



**1.0 UTANGULIZI**

Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (Tume) ilianzishwa mwaka 1980 kwa Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura ya 171. Kwa mujibu wa Sheria hii pamoja na majukumu mengine, Tume ina majukumu ya kupitia na kutathmini utekelezaji wa sheria zote za Jamhuri ya Muungano kwa lengo la kuziwezesha sheria hizo kuendana na mabadiliko yanayotokea katika nyanja za kijamii, kisiasa, kiuchumi, kisayansi na teknolojia. Aidha, Tume ina jukumu la kutoa elimu ya sheria kwa umma.

**2.0 MAZAO YA UHALIFU**

Mazao ya uhalifu ni fedha, faida au mali zinazopatikana wakati au baada ya kutenda uhalifu. Watuhumiwa wa uhalifu baada ya kukamatwa na kupelekwa mahakamani, na kutiwa hatiani mali walizojipatia wakati wanatenda uhalifu au baada ya uhalifu ni lazima zitaifishwe kwenda Serikalini.

**3.0 UMUHIMU WA KUTAIFISHA MAZAO YA UHALIFU**

Utaifishaji wa zao la uhalifu unafanyika ili kuifundisha jamii kuwa uhalifu haulipi. Adhabu za kawaida hazitoshelezi kutokomeza uhalifu hasa katika makosa ya uhalifu wa kupangwa, sababu wahalifu walio kwenye magenge uhalifu hata wakimaliza

kutumikia vifungo vyao wana uhakika wa kupata mazao yao ya uhalifu na huyatumia kuendeleza uhalifu. Hivyo ni muhimu kwa wahalifu kutaifishiwa mapato ya uhalifu kwa kuwa wahalifu wanaumia zaidi pale mali zao
;
zinapotaifishwa kuliko kutumikia adhabu kifungo.

Utaifishaji wa mapato ya uhalifu ni mkakati muhimu kwa kuwa unazuia uhalifu kwa kuondoa matamanio ya kufanya uhalifu kwa kuwa mhalifu anafahamu kuwa ikiwa atakamatwa hataweza kufaidia na vitendo vya uhalifu.

**3.0 SHERIA ZINAZORATIBU MAZAO YA UHALIFU**

- Sheria ya Mazao ya Uhalifu Sheria (Sura ya 256)
- . Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (Sura ya 20)
- Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa (Sura ya 200)
- Sheria ya Wanyamapori, (Sura ya 283); na
- Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, ( Sura ya 329).

Sheria hizi zinaipa mamlaka Mahakama pamoja na adhabu nyingine kuamuru kifaa kilichotumika kufanyia uhalifu au mali iliyopatikana kutokana na uhalifu kutaifishwa na kwenda Serikalini.

**4.0 MAMLAKA YA MAHAKAMA KUTAIFISHA MAZAO YA UHALIFU**

Endapo mshitakiwa ametiwa hatiani kwa kosa kubwa, Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza kuiomba mahakama amri ya kutaifishaa mali yoyote inayohusiana na uhalifu aliyoshitakiwa nao, amri ya kutwaa mali yoyote yenye thamani inayotakiwa au amri ya malipo dhidi ya mtu yeyote aliyefaidika kutokana na kitendo cha kihalifu.

Mkurugenzi wa Mashtaka anatakiwa kutoa notisi ya maandishi ndani ya siku 30 kwa mtu yeyote au watu ambao anadhani wana maslahi na mali inayotakwa kutaifishwa. Baada ya kupewa notisi mtu mwenye maslahi atatakiwa awepo siku ya usikilizaji wa kesi, na atoe ushahidi jinsi ambayo mali husika inamhusu. Baada ya kusikiliza maombi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya kuomba kutaifisha mazao ya uhalifu na kujiridhisha, Mahakama itatoa amri ya kutaifisha mali hizo kuwa za Jamhuri ya Muungano.

Kuna mazingira ambayo mali zilizopatikana katika uhalifu zinakuwa hazijulikani zilipo hata baada ya uchunguzi yakinifu kufanyika kutokana na;

- Mali hizo kuhamishwa umiliki au kuuzwa kwa mtu mwingine ambaye hakujua ni mazao ya uhalifu;
- Mali hizo zimepelekwa nje ya nchi na haziwezi kurudishwa
- Thamani ya mali hizo kushuka au;
- Mali husika kujumuishwa na mali za mtu mwingine na kuleta ugumu kuzitenganisha.

Mahakama ina mamlaka ya kutoa amri ya kutaifisha mali nyingine ya mshtakiwa yenye thamani sawa na mali iliyopatikana kutokana na uhalifu.

Mtu yeyote ambaye hajaridhika na uamuzi wa kutwaa na kutaifishwa kwa mali anaweza kuomba "amri ya zuio" ndani ya miezi 6 tangu mahakama itoe amri. Zuio la kutaifisha mali lisipofunguliwa ndani ya miezi 6, mali hiyo itataifishwa.